BARAZA LA WAWAKILISHI

ZANZIBAR

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA UCHUMI NA UWEKEZAJI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KAZI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

----------------

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 124 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar Toleo la Februari, 2024]*

May, 2026

# 1.0 SEHEMU YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** hatuna budi kumshukuru Allah mwingi wa Rehma na ambae kwake tunahitaji kurehemewa, Allah ambae ametupa neema ya uhai hadi leo tunapumua vyema tukiwa na afya tele, hivyo hatuna budi kusema *Alhamdulillah.*

**Mheshimiwa Spika,** tunamshukuru pia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake imara na thabiti unawaletea maendeleo ya haraka wananchi wa Zanzibar.

**Aidha,** naomba pia kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar kwa uongozi, hekima, busara na uweledi katika kuliendesha Baraza hili Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza ya Uchumi na Uwekezaji ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii.

Kwa upendo mkubwa naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za Hansard ya Baraza kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| i. | Mhe. Makame Mohammed Sufiani | Mwenyekiti |
| ii. | Mhe Dr. Mahmoud Omar Mohammed | M/Mwenyekiti |

| | | |
|---|---|---|
| iii. | Mhe. Alley Masoud Alley | Mjumbe |
| iv. | Mhe. Shafi Mohammed Shafi | Mjumbe |
| v. | Mhe. Chumu Kombo Khamis | Mjumbe |
| vi. | Mhe. Tabia Maulid Mwita | Mjumbe |
| vii. | Mhe. Toufiq Salim Turky | Mjumbe |
| viii. | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |
| ix. | Ndg. Abdu Maulid Haji | Katibu |
| x. | Ndg. Shaaban Suleiman Juma | Afisa Bajeti |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe.Shariff Ali Shariff (MBM) Waziri wa Uchumi na Uwekezaji kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake kwa ufanisi. Aidha, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu yangu Khamis Suleiman Mwalim na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Rashid Ali Salim pamoja na Mkurugenzi wa ZIPA Ndugu yangu Saleh Saad Mohammed kwa kazi nzuri wanayofanya kumsaidia Mheshimiwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Toleo la Februari, 2024, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Uchumi na Uwekezaji ya Baraza la Wawakilishi, Zanzibar Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya

Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 124(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

- **i.** Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya Utangulizi pamoja na kuelezea msingi iliyotumika katika uandaaji wa Taarifa hii pamoja na namna Kamati Uchumi na Uwekezaji ilivyofanya kazi;
- **ii.** Sehemu ya Pili imebeba taarifa ya uchambuzi wa kina juu ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
- **iii.** Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii inaonyesha uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
- **iv.** Sehemu ya Nne imebeba maoni pamoja na ushauri wa Kamati baada ya uchambuzi yakinifu uliofanyika; na
- **v.** Sehemu ya Tano ni hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuaji wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa uchambuaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji unatokana na matakwa ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, 2024. Kanuni ya 119(3) zinaipa Kamati hii miongoni na majukumu mengine, jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Aidha, Kanuni ya 101 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar Toleo la mwaka 2024 imeweka masharti yanayoelekeza kuwa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati ya Uchumi na Uwekezaji kabla ya kujadiliwa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

Hivyo, naomba kulijulisha Baraza lako tukufu kuwa masharti hayo yaliyoelekezwa katika Kanuni zetu za Baraza yamezingatiwa na kwamba naliomba Baraza lako Tukufu liijadili hoja ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji pamoja na Taarifa hii ya Kamati ya Uchumi na Uwekezaji.

### 1.3 Maeneo ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji inagusa Fungu moja Nambari **006** lenye Programu Kuu tatu (3) ambazo ni;

- **i.** Programu Kuu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Upatikanaji wa Ajira
- **ii.** Programu Kuu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini
- **iii.** Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji

na Programu Ndogo nane (7)

Naomba kutoa taarifa mbele ya Baraza lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Programu zote tatu pamoja na Programu ndogo zilizoambatana na Programu Kuu tarehe 21 April 2026.

## 2.0 TAARIFA YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA WIZARA YA KAZI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi unaweka msingi ya Kikanuni kwa Kamati hii kutoa ushauri unaohusiana na Hoja hii ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji. Uchambuzi wetu ulijielekeza katika maeneo makuu manne yafuatayo; -

i. Makusanyo ya mapato;
ii. Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoishia 2025/2026;
iii. Muelekeo wa Wizara katika bajeti ya 2026/2027; na
iv. Utekelezaji wa maagizo ya Kamati.

### 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Kazi na Uwekezaji ililenga kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **7,209,087,725** kupitia vyanzo mbalimbali chini ya Wizara hiyo.

Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2026 Wizara ya Kazi na Uwekezaji imeweza kukusanya jumla ya Shilingi za Kitanzania **4,819,133,207** sawa na **Asilimia 72** ya malengo yaliyokusudiwa. Mapato hayo yalipatikana kwa utaratibu ufuatao:-

i. Ada za Usajili wa Vyama vya Ushirika TZS**. 35,023,000**

ii. Ada za Ukaguzi wa vyama vya Ushirika **TZS. 18,955,000**

iii. Ada za Ukaguzi wa usalama na afya maeneo ya kazi **TZS 280,390,000**

iv. Ada za Uthibitisho wa Mikataba TZS**. 375,315,607**

v. Ada za uhakiki wa Mikataba **TZS. 133,660,000**

vi. Kibali cha kufanyakazi kwa wasiokua raia **TZS. 3,975,789,600**

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo;

i. Kati ya vyanzo vyote vilivyoainishwa hapo juu ni Kamisheni ya Kazi tu katika uthibitisho wa mikataba ya kazi imeweza kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2025/2026 kwa kufikia **Asilimia 110.5** kwa ujumuisho wa Unguja na Pemba hadi kufikia Machi 2026.
ii. Kamisheni ya Kazi kupitia makusanyo ya ada za vibali vya wageni wameweza kuvuka malengo kwa kupata **Asilimia 119.2** hadi kufika Machi, 2026
iii. Uhaba wa Mikataba inayohusisha ajira za nje umepelekea Idara ya Ajira kushindwa kufikisha malengo kwa kukusanya **Asilimia 49.5** hadi kufikia Machi, 2026

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umebaini kuwa mwenendo wa makusanyanyo katika vyanzo vyengine si wa kuridhisha na kupelekea kubaki chini ya **Asilimia 40** hadi kufika Machi, 2026. Mfano; Ada ya ukaguzi

wa usalama na afya katika maeneo ya kazi imekusanya **Asilimia 19.9 tu** kwa mapato ya Unguja na Pemba, na ada ya ukaguzi wa vyama vya ushirika imepatikana **Asilimia 11.7** kwa mjumuisho wa Unguja na Pemba.

Katika uchambuzi uliofanyika, kamati imegundua sababu mbalimbali zilizopelekea vyanzo vyengine vya Wizara hii kushindwa kufikisha malengo ya makusanyo ya mapato kama ifuatavyo;

a. Ukosefu wa usafiri na vitendea kazi kwa Idara ya Usalama na Afya Kazini
b. Upungufu wa wanyakazi na vitendea kazi uliojitikozea kwa Idara ya ushirika
c. Kuhamishwa kwa Idara ya Ushirika kwenda Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji

### 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Kazi na Uwekezaji iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 28,700,300,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo Shilingi 15,000,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, Shilingi 7,815,700,000 kwa ajili ya mishahara na Shilingi 5,125,124,293 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2026 Wizara ya Kazi na Uwekezaji ilipokea jumla Shilingi 10,081,077,681 sawa na **asilimia 48** ya fedha iliyoidhinishwa na Baraza lako Tukufu kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

kati ya fedha hizo, Shilingi 5,222,883,882 kwa ajili ya mishahara, Shilingi 1,327,680,394 kwa matumizi ya kawaida, Shilingi 3,468,642,861 kwa Mradi wa Maendeleo Fumba na Shilingi 175,969,250 kwa malipo ya fidia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi wa Kamati hii umebaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya Wizara si wa kuridhisha hali ambayo inapelekea Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa kwa mwaka husika wa fedha. Hivyo, ni rai ya Kamati hii kuiomba Serikali katika kipindi hiki kilichobaki kuiwezesha vyema Wizara hii kupitia fungu la 006 ili kukamilisha na kuyafikia malengo yaliyopangwa mwaka huu wa fedha 2025/2026.

### 2.4 Uchambuzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika Bajeti ya mwaka unaoishia, jumla ya Shilingi 3,468,642,861 zimeweza kupatikana kwa ajili ya Mradi wa Maendeleo Fumba, hata hivyo, Kamati kwa mashirikiano na Wizara inashauri kufanyika ziara maalumu katika mradi huo ili tuone uhalisia wa fedha iliyotumika. Kamati imebaini kuwa fedha hizo zimeweza kutumika katika kuanza matengenezo ya miundombinu ya barabara ya kilomita 8 za barabara za ndani katika eneo la Fumba.

### 2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni,

ushauri na mapendekezo mbali mbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima naomba kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba Wizara hii chini ya Usimamizi wa Mheshimiwa Waziri makini *Komredi Shariff Ali Sharif,* ilitekeleza kwa kiwango kikubwa maoni na ushauri uliokuwa unatolewa na Kamati kwa nyakati tofauti ikiwa ni pamoja na kuyachukua mapendekezo ya kamati hii kuwa nyenzo ya utekelezaji wa kazi zake endelevu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Kazi na Uwekezaji, inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya Shilingi 8,500,000,000 ikilinganishwa na Shilingi. 7,209,087,725 katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.
Aidha, makadirio ya ukusanyaji wa mapato katika Wizara hii yameongezeka kwa Shilingi 1,290,912,275 sawa na **asilimia 15** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya mapato kwa mwaka 2025/2026. Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vinne (4) Ada za usajili, Ada za mikataba ya ajira za ndani na nje, Ada za Vibali vya Kazi kwa Wasio Raia na Ada za Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi wa mapato hayo, Kamati ilihoji na kutaka kujua sababu ya kuongezeka kwa makisio ya mapato

ambapo ilibainika kuwa ni kutokana na kuongezeka na kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inaajiri wageni na Wazanzibari wengi. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Kazi na Uwekezaji kuwa na mashirikiano ya karibu na Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji ili kwa pamoja waweke mikakati thabiti ya kuwaunganisha Wazanzibari na fursa za ajira nje ya nchi pamoja na kuweka mfumo madhubuti wa kukusanya mapato kwa yatokanayo na ujira kwa Wazanzibari wanaofanya kazi nje ya nchi ili kuongeza mapato.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na ongezeko la makadirio ya makusanyo hayo Kamati imebaini kuwa, Wizara inaweza kukusanya zaidi ya kiwango kilichokadiriwa kutokana na ongezeko kubwa la wafanyakazi wa kigeni wanaendelea kuingia Nchini pamoja na ongezeko la miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo mahoteli, ujenzi wa miundombinu, ujenzi wa majengo mbalimbali ya kibiashara na kadhalika. Hivyo, Kamati imeishauri Wizara kuangalia uhalisia wa maendeleo ya Nchi badala ya kujishusha katika makadirio ya mapato yako jambo ambalo litapunguza spidi ya ukusaji pale ambapo makusanyo yatapita malengo yaliyoekwa sasa.

Aidha, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inatarajia kukusanya jumla ya TZS 4.09 bilioni kutoka vyanzo vyake vya mapato.

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Kazi na Uwekezaji, **(Fungu 006)** imetengewa jumla ya **TZS. 27,091,580,000** Kati ya fedha hizo **TZS. 6,873,280,000** ni Mishahara; **TZS. 5,218,300,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; **TZS 15,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imekadiriwa kutumia Jumla ya **TZS 22,655,000,000** kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwa Bajeti ya fedha za Mishahara katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 zimepungua kwa **Shilingi 936,420,000** sawa na **asilimia 11** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha. Aidha, fedha za matumizi ya kawaida zimepungua kwa **Shilingi 666,300,000** sawa na **asilimia 11**. Fedha za Maendeleo zimeendelea kubaki vilevile.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kupungua kwa Bajeti ya fedha za Mishahara na Matumizi ya Wizara kumetokana na kuhamishwa kwa baadhi ya taasisi kupelekwa katika Wizara Mpya iliyoundwa Wizara ya Ajira, Vijana na Uwezeshaji.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutokupunguza fedha za Maendeleo ili kuiwezesha Wizara kutekeleza Miradi mbalimbali iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti katika fungu hili ili kuendana na uhalisia wa maendeleo yanayoendelea kwa kasi Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za maendeleo ili Wizara hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kufuatia uchambuzi wakina uliyopelekea majadiliano ya yakinifu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Kamati hii inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu ya Programu zote kama ifuatavyo: -

i. Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo ya Mapato kwa baadhi vyanzo si wa kuridhisha. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya wafanyakazi katika sekta zenye watendaji hafifu pamoja na kuwapatia vitendea kazi ili kuongeza mapato ya Wizara.

ii. Kutenganishwa kwa vyanzo vya Mapato vilivyounganishwa katika Kasma ya Kamisheni ya Kazi Nambari **1422012** ambayo imeunganyisha vyanzo vifuatavyo;

   a. Chanzo cha Mapato yanayopatikana katika malipo ya mashauri mbalimbali yanayofunguliwa DHU, na

   b. Chanzo cha Mapato yanayotokana na vibali vya wafanyakazi wanaoenda nje ya nchi.

iii. Kutopatikana kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ndani ya wakati stahili kuna sababisha kusuasua kwa utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha ni vyema kwa Serikali kujielekeza zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikanaji wa fedha za Wahisani wa Maendeleo ni wa kusuasua.

iv. Kutopatikana kwa fedha zinazohitajika kukamilisha miradi mbali mbali yenye malengo ya kuweka mazingira mazuri na salama yatakayovutia wawekezaji ndani na nje ya nchi kutapelekea Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kushindwa kufikia malengo kwa wakati. Kutokutimizwa kwa miradi hiyo ndani ya wakati, kutapelekea Serikali kukosa mapato kupitia wawekezaji mbalimbali.

v. Mradi wa maeneo ya Uwekezaji Micheweni ni moja ya miradi inayosimamiwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ambayo kukamilika kwake kutainyanyua Pemba kiuchumi kwa kupunguza tatizo la ajira kwa vijana pamoja na kuingizia mapato mengi Serikalini. Hata hivyo, Kamati imebaini kusuasua kwa Mradi huo kunakotokana na ukosefu wa fedha zinazohitajika kukamilisha miundombinu inayohitajika. Hivyo, tunaiomba Serikali yetu sikivu kukamiisha fedha inayohitajika ili Mradi huo kumalizika kabla ya Wananchi hawajavamia maeneo yale na kusababisha hasara kubwa kwa Taifa.

vi. Mradi wa kuyaendeleza maeneo huru ya viwanda vidogovidogo

yaliyopo Amani ni muhimu kwa ustawi wa wazalishaji wa ndani. Kamati imebaini uchakavu wa baadhi ya miundombinu unaoleta usumbufu kwa wafanyabiashara waliopewa maeneo hayo. Aidha, ufinyu wa nafasi katika maeneo hayo ni miongoni mwa changamoto kubwa zinaleta kilio kwa wawekezaji waliopo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza fedha zaidi kupitia ZIPA kuyaendeleza maeneo hayo ili kuleta tija na kuongeza mapato.

vii. Kamati inashauri Wizara kuliweka suala la ufuatiliaji wa migogoro ya Ardhi iliyotengwa kwa shughuli za Uwekezaji, kuwa ni miongoni mwa Vipaumbele vya Wizara. Hatua hiyo itaiwezesha serikali kuwa na maeneo yanayotambulika kisheria.

viii. Kamati inashauri Wizara kupitia ZIPA kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa fedha ili kuanza kwa harakati za kuliwekea uzio shamba la Makurunge lililopo katika Wilaya ya Bagamoyo. Kamati ilishuhudia uvamizi wa kasi unaoendelea katika Shamba hilo licha ya ulinzi unaosimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo.

ix. Kamati inaishari Serikali kuharakisha upatikanaji wa fedha ili kuiwezesha Wizara kukamilisha mchakato wa uhuishaji wa Kampuni ya Uwekezaji Zanzibar. Ukamilikaji wa Kampuni hii, kutaiwezesha Serikali kuingia katika soko la uwekezaji kwa kununua hisa pamoja na kuwekeza katika maeneo mbalimbali.

x. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha mchakato wa kuifanyia mabadiliko Sheria ya Ajira Namba 11 ya 2005 ili kuweza kuondosha

maingiliano ya kiutendaji baina ya Wizara hii na Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. Aidha, tunashauri kuwepo kwa Sheria ya Kazi ambayo itajikita zaidi katika kulinda viwango vya kazi ikiwemo stahili, mikataba na mengineyo.

xi. Tunaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya kutosha ya Idara ya Usalama na afya kazini (OSHA) ili waweze kuajiri watendaji zaidi pamoja na kuongeza vitendea kazi vya kuwawezesha kufanya kazi ya kuisaidia Zanzibar katika eneo la usalama wa wafanyakazi na pia itawezesha Idara kuongeza kasi ya kukagua maeneo mengi ya kazi Nchini. Kutekelezwa kwa ushauri huu kutapelekea Wizara kuongeza mapato zaidi.

## 5. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba tena kuchukua fursa hii kumshukuru Muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kunijaalia mimi mwenyewe na wengine wote pumzi na nguvu ya kuwepo katika Baraza lako hili tukufu. Aidha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi na kunivumulia kuwasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Aidha, bado tunaendelea kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar, Dr. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Msaidizi wake Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika Zanzibar, hakika ile dhana ya *yajayo ni neema zaidi* inaenda kutimia kwa kishindo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Uchumi na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Ahsante

……………………………………

Mhe. Makame Mohammed Sufiani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi na Uwekezaji,

Baraza La Wawakilishi,

**Zanzibar.**